



RIPOTI YA KIHAIIDROLOJIA JARIDA LA MWEZI

BWAWA LA MTERA

JULAI, 2026

Tarehe ya Utekelezaji: 24 Nov 2025
Toleo, No: 00



"KILA TONE LINATHAMANI"


Tarehe ya Utekelezaji: 24 Nov 2025
Toleo, No: 00

Muhtasari wa Hali ya Maji

Bwawa la Mtera hupokea maji kutoka kwenye mito mikuu mitatu ya Great Ruaha, Little Ruaha na Kizigo, ambayo yote ipo ndani ya kidakio cha Mto Great Ruaha. Mito hii ina mchango mkubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kuwezesha uzalishaji wa umeme wa maji, kusaidia shughuli za kilimo cha umwagiliaji, kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa matumizi ya majumbani, viwandani na mifugo, pamoja na kuhifadhi mtiririko wa mazingira unaohitajika kwa uhai wa mifumo ikolojia na ustawi wa maeneo yaliyopo chini ya mkondo wa mto.

Hadi kufikia mwishoni mwa Julai 2026, mtiririko wa maji unaoingia katika Bwawa la Mtera ulikuwa sawa na asilimia 95 ya wastani wa muda mrefu (Long-Term Average – LTA) wa mwezi huo, hali inayoashiria kuwa upatikanaji wa maji ulikuwa katika kiwango cha kawaida. Hali hii ilitokana na mvua zilizonyesha kwa kiwango cha wastani katika maeneo ya juu ya kidakio, sambamba na usimamizi madhubuti wa rasilimali za maji uliofanyika katika Bonde la Rufiji.

Katika kipindi chote cha Julai 2026, kina cha maji katika Bwawa la Mtera kiliendelea kuwa juu ya wastani wa muda mrefu (Long-Term Average – LTA) wa mwezi husika. Kufikia tarehe 31 Julai 2026, kina cha maji kilifikia mita 697.76 juu ya usawa wa bahari (MASL), sawa na asilimia 100.57 ya wastani wa muda mrefu wa mwezi Julai.



Hali ya Hewa

Hali ya Mvua – Julai 2026:

Taarifa za mvua zinaonesha kuwa Kidakio cha Great Ruaha kilirekodi hali ya ukavu katika kipindi chote cha Julai 2026. Kutokana na hali hiyo, ili sababisha kupungua kwa ujazo wa maji yanayoingia katika mito na vijito, hususan vile vinavyotegemea mvua za msimu kama chanzo kikuu cha mtiririko wake.


Mwelekeo wa Hali ya Hewa – Agosti 2026:

Kwa mujibu wa utabiri wa hali ya hewa uliotolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA):


Maeneo mengi ya Bonde la Rufiji yanatarajiwa kuendelea kuwa na hali ya ukavu katika kipindi chote cha Agosti 2026.

Wiki ya Kwanza	Wiki ya Pili	Wiki ya Tatu	Wiki ya Nne
Halia ya ukavu kwa ujumla	Halia ya ukavu kwa ujumla	Halia ya ukavu kwa ujumla	Halia ya ukavu kwa ujumla


Utabiri wa Mvua
Wiki 01 Agosti, 2026




Utabiri wa Mvua
Wiki 02 Agosti, 2026



Utabiri wa Mvua
Wiki 03 Agosti, 2026



Utabiri wa Mvua
Wiki 04 Agosti, 2026



Hali ya Mtiririko wa Maji

Vituo vya Kihaidrolojia



Kwa ujumla, wastani wa mtiririko wa maji katika mito wakati wa Julai 2026 ulifikia asilimia 95 ya wastani wa muda mrefu (Long-Term Average – LTA) wa kipindi cha mwaka 2000–2025, hali inayoonesha kuwa mtiririko wa maji ulikuwa katika kiwango cha kawaida. Jedwali 1 linaelezea mchanagnuo wa takwimu za wingi wa maji katika mito inayoingiza maji katika bwawa la Mtera.

Jedwali 1: Mchanganuo wa Takwimu za Wingi wa Maji


Na.	Namba ya Kituo	Mto	Wastani Wingi wa Maji (m3/s) Julai 2026	Wastani Wingi wa Maji -LTA (Julai) 2000-2025	Maelezo
1	1KA59	Great Ruaha at Msembe	3.7	6	Chini ya Wastani
2	1KA31	Little Ruaha at Mawande	24.7	13.3	Juu zaidi ya Wastani
3	1KA42A	Kizigo at Chinugulu	4.5	11.9	Chini zaidi ya Wastani

Matokeo ya Kihidrolojia

Hali ya kihaidrolojia katika kidakio cha Great Ruaha wakati wa mwezi Julai 2026 ilitawaliwa na kupungua kwa mtiririko wa maji katika mito kutokana na hali ya ukavu iliyoendelea kujitokeza. Hata hivyo, Mto Mdogo wa Ruaha katika kituo cha Mawande uliendelea kurekodi mtiririko wa maji uliokuwa juu ya wastani wa muda mrefu, licha ya hali ya ukavu iliyokuwepo



Hali ya Maji Bwawani



Kufikia mwisho wa mwezi Juni 2026:

- Hali ya usawa wa maji katika bwawa la Mtera iliendelea kuwa juu ya kiwango cha maji cha uzalishaji umeme (Maximum Operational Level)
- Usawa wa maji ulifikia mita 697.76 juu ya usawa wa bahari (masl), sawa na asilimia 100.57 ukilinganisha na wastani wa muda mrefu kwa mwezi Julai.

Uchambuzi

- Licha ya kupungua kwa wingi wa maji yanayoingia katika Bwawa, kiwango cha maji kilibaki juu ya wastani wa muda mrefu.
- Hali hii imedhihirisha usimamizi thabiti wa matumizi ya maji na operesheni ya bwawa katika uzalishaji umeme.

Mapendekezo

- Inapendekezwa uendeshaji wa Mabwawa unapaswa kuendelea kufuata miongozo na taratibu zilizowekwa ili kuhakikisha kiwango cha maji kinachohifadhiwa kinatosheleza mahitaji ya uzalishaji wa umeme wa maji pamoja na matumizi mengine ya rasilimali za maji.
- Inapendekezwa katika kipindi cha kiangazi, watumiaji wote wa maji wanapaswa kuzingatia masharti na viwango vya uchukuaji wa maji vilivyobainishwa katika vibali vya matumizi ya maji walivyopewa, ili kuhakikisha matumizi endelevu na usimamizi bora wa rasilimali za maji zilizopo.

